

MOLA WETU SAMAHANI

1. Kwa jina lake manani,
Subhana Buruhani,
Nipate kaa kitini,
Nandike karatasini,
Haya ninayo wazia.
2. Arahimu Rahmani,
A'lhayu Qayumuni,
Yako kwake mkononi,
Ardhi na ya mbinguni,
Ngoja nikuhadithia.
3. Hakimu wa Kiyamani,
Dunia na akherani,
Ajua ya Uwanjani,
Na yaliyo mafichoni,
Asiye kupendelea.
4. Sote tumo amrini,
Nyama nao ikhiwani,
Alitakalo Enzini,
Hana wa kumhini,
Yote yanatimia.
5. Bora tuwe utiini,
Amrize tufatani,
Tujengizwa peponi,
Tunusurike motoni,
Mwenyewe akijalia.
6. Huyo ni Mola amini,
Mwingine hawafanani,
Asiye ushirikani,
Hangii usingizini.
Tafadhalini sikia.
7. Jamani sikilizeni,
Wote nawaombeni,
Tusijitie dhambini,
Kujifanya majinuni,
Bure tutaangamia.
8. Yailahi tujalieni,
Tuipate samahani,
Tupewe na afueni,
Hali yetu taabani.
Zidi kutuhurumia.
9. Yote tuzingatieni,
Sana tuyafikirini,
Tuyahifadhi moyoni,
Na kukinga kifuani.
Yasipate kuachia.
10. Kumi nangia ndani,
Nauacha usukani,
Nimefika ukingoni,
Naiomba samahani.
Kama nimekosea.

*Yusuf M. Kalala.
Washington, D.C.
September 19, 2002*